(SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA, (MAMLAKA ZA WILAYA)

(SURA YA 287)

SHERIA NDOGO

Zimetungwa chini ya kifungu cha 153

SHERIA NDOGO ZA (USHURU WA WA MAZAO YA KILIMO NA MATUNDA) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA IRINGA, 2017

			SEHEMU YA KWANZA UTANGULIZI
Jina na mwanzo wa kutumika	1		Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za Halmashauri ya wilayaya Iringa (Ushuru wa Mazao ya Kilimo na Matunda) za mwaka 2017 na zitaanza kutumika baada ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.
Matumizi	2		Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote la Mamlaka ya Halmashauri ya wilaya ya Iringa.
Tafsiri	3		Katika Sheria Ndogo hizi isipokuwa pale itakapoelezwa vinginevyo: **"Afisa Mtendaji" Afisa Mtendaji wa Kata au Kijiji au Afisa mwingine atakayeidhinishwa kusimamia utekelezaji wa sheria Ndogo hizi kwa nafasi hiyo** **"Afisa muidhiniwa" Maana yake ni Mweka Hazina wa halmashauri au Afisa mwingine atakayeidhinishwa kusimamia utekelezaji wa sheria Ndogo hizi.** **"Mazao" Maana yake ni mazao ya kilimo na matunda yanayozalishwa au kusafirishwa kupitia eneo la Halmashauri** **"Chakula cha Binadamu" Maana yake ni kila kitu kitumikacho kwa chakula au kinywaji kwa binadamu.** **'Duka" Maana yake ni jengo lolote ambapo shughuli ya kununua na kuuza bidhaa mbalimbali zinafanyika hapo.** **"Halali" Maana yake uzito, Urefu na Ujazo wowote,**

			kipimo, kipimio au kifaa chochote cha kupimia ambacho hakina makosa zaidi ya kiwango kilichoamuliwa. **"Halmashauri" Maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Iringa .** **"Gulio" Maana yake ni sehemu au eneo ambalo limetengwa kwa shughuli za kuuza na kununua mazao.** **"Lumbesa" Maana yake ni ujazo unaozidi uzito halali wa zao au bidhaa husika.** **"Mahakama" Maana yake ni Mahakama ya ngazi yoyote na italihusisha pia Baraza la Kata.** **"Mkurugenzi" Maana yake ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashuri ya wilaya ya Iringa.** **"Mnunuzi" Maana yake ni mtu, taasisi, kampuni au kikundi chochote kinachojishughulisha na ununuzi wa mazao au bidhaa nyingine katika eneo la Halmashauri.** **"Muuzaji" Maana yake ni mtu, taasisi, kampuni au kikundi chochote kinachojishughulisha na uuzaji wa mazao au bidhaa nyingine katika eneo la Halmashauri.** **"Soko" Maana yake ni sawa na ile ya gulio** **"Uzito, Urefu na Ujazo Halisi" Maana yake ni uzito, urefu au ujazo wa kitu chochote kuondoa uzito wa kihifadhio au kifungashio chake.** **"Wakala" Maana yake ni wakala wa kukusanya ushuru anayefanya kazi hiyo kwa niaba ya Halmashauri**. **"Wakala wa Vipimo" Maana yake ni wakala wa vipimo kwa Mujibu wa Sheria ya Vipimo Sura ya 340**
			SEHEMU YA PILI WAJIBU WA HALMASHAURI
Wajibu wa Halmashauri	4		Katika kuhamasisha na kutekeleza azma ya ukusanyaji mapato ya Halmashauri,kuzingatia vipimo na vifungashio sahihi katika biashara za mazao Halmashauri itakuwa na wajibu wa:- (a) Kuhakikisha viongozi wa serikali, vyama vya siasa na wadau wengine wanashiriki ipasavyo katika

			kuelimisha jamii juu ya matumizi sahihi ya vipimo na vifungashio kwenye biashara za mazao mbalimbali katika Halmashauri. (b) Kumuwezesha wakala kukusanya ushuru kwa kutumia vitabu halali vya Halmashauri (c) Kuweka mabango kwenye kila kijiji yanayohamasisha matumizi ya vipimo na vifungashio sahihi katika biashara za mazao mbalimbali. (d) Kuanzisha Soko au Gulio katika kila kijiji (e) Kuhakikisha upatikanaji wa vipimo na wahakiki wa vipimo. (f) Kumpa ushirikiano Wakala katika utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi na kutoa msaada wa Kisheria pale itakapohitajika
Wajibu wa serikali ya kijiji	5		Serikali ya kijiji itakuwa na wajibu ufuatao:- (a) Itatenga ardhi kwa ajili ya Soko au Gulio. (b) Kwa kushirikiana na uongozi wa kitongoji itahakikisha kuwa kila mkazi na asiyemkazi anauzia au kununua mazao kwenye Soko au Gulio. (c) Kwa kushirikiana na uongozi wa kitongoji itakuwa na wajibu wa kuhakikisha kuwa mazao yote yanauzwa kwa vipimo na vifungashio vilivyokubaliwa. (d) Kuhakikisha kwamba kila mnunuzi wa mazao ananunua mazao kwa kipimo na vifungashio sahihi kulingana na zao analonunua. (e) Kuhakikisha kwamba kila muuzaji anakua na kipimo na kifungashio sahihi kulingana na zao analouza.
Wajibu wa Afisa muidhiniwa	6	1	Afisa mwidhiniwa atakua na wajibu wa kuhakikisha kwamba:- (a) Vipimo sahihi na vyenye ubora uliokubalika vinatumika katika biashaza za mazao. (b) Mazao yote yanauzwa na kununuliwa kwenye Gulio au Soko. (c) Eneo la Gulio au Soko lina mzani halali kwa ajili ya kupimia bidhaa za mazao zinazouzwa katika eneo hilo. (d) Viwango halali vya ushuru vinatozwa kwa kila mfanyabiashara bila udanganyifu wa aina yeyote
		2	Itakuwa ni halali kwa Afisa muidhiniwa kusimamisha gari au chombo chochote cha uchukuzi na kukagua ili kutekeleza masharti ya Sheria Ndogo hizi ikiwa ni pamoja na kukagua uzito, urefu na ujazo wa mazao na risiti zilizotolewa kwa malipo yaliyolopwa
		3	Itakuwa ni halali kwa Afisa muidhiniwa kuingia katika Duka au Soko kwa lengo la kukagua uhahali wa vipimo na

			vifungashio vya mazao.
		4	Mtu yeyote atakayemzuia Afisa muidhiniwa, baada ya kujitambulisa, katika kutekeleza majukumu yake chini ya Sheria Ndogo hizi au kutoa taarifa ambazo anajua si za kweli atakuwa ametenda kosa.
			SEHEMU YA TATU UANZISHWAJI WA GULIO/SOKO
Gulio/Soko	7	1	Kila kijiji kinatakiwa kuanzisha Gulio/Soko kwa mazao.
		2	Ni marufuku kwa mnunuzi yeyote kununua mazao katika maeneo ambayo sio Gulio au Soko la kijiji husika.
		3	Ni marufuku kwa muuzaji yeyote kuuzia mazao yake maeneo ambayo sio Gulio au Soko.
		4	Mauzo yote ya mazao ya kilimo yatakuwa yanafanyika kama ilivyoelekezwa na Sheria Ndogo hizi.
		5	Bidhaa za mazao ambazo ni maalum kwa matumizi madogomadogo ya nyumbani yanaweza kuuzwa katika eneo la makazi la muuzaji.
		6	Ni marufuku kwa mazao kuuzwa kwa kipimo kisicho halali, kama vile lumbesa.
Ukaguzi wa Magari	8		Halmashauri itatenga maeneo katika vijiji kwa ajili ya kukagua magari yaliyobeba mazao endapo ushuru halali umelipwa au haukulipwa na kuamuru hatua stahiki zichukuliwe juu ya udanganyifu utakaokuwa umejitokeza ikiwa ni pamoja na kuamuru gari ipelekwe yard ya Halmashauri na kumtaka dereva na mwenye mzigo kulipa faini isiyozidi elfu hamsini (50,000) kwa kila gunia litakalokuwa limezidisha uzito.
			SEHEMU YA NNE VIFUNGASHIO/VIPIMO VYA MAZAO MBALIMBALI NA USHURU
Vipimo na vifungashishio vya mazao mbalimbali na ushuru wa mazao	9	1	Bila kuathiri vifungu vingine vya Sheria Ndogo hizi Mazao yote yatauzwa kwa: - (a) Uzito, Urefu na Ujazo kama ilivyoainishwa katika jedwali la kwanza (b) Uzito, Urefu na Ujazo Halisi, Kama ilivyoainishwa katika jedwali la pili. (c) Kuwekwa vitambulisho vikionyesha uzito, ujazo au urefu halisi kwenye vifungashio au vihifadhio.
		2	Kifungu cha 8 (1) hakitahusika kwa: - (a) Mazao yoyote yale yanayouzwa eneo la makazi ya muuzaji na ambayo ni maalum kwa matumizi madogomadogo ya nyumbani mfano upangaji nyanya kwenye mafungu.

			(b) Mazao yoyote yale yanayouzwa kwa kiwango kisichozidi gramu 50 au mililita 50. (c) Ushuru wa Mazao itakuwa ni asilimia isiyozidi tano (50) ya bei ya manunuzi kwa kila kifungashio kama vile gunia na vifungashio vingine (d) Malipo halisi ya ushuru yatategemea maamuzi ya Halmashauri ili mradi isizidi asilimia tano ya bei ya manunuzi kwa kila kifungashio na maamuzi ya halmashauri yatahesabika kuwa sehemuya sheria ndogo hizi
		3	Upimaji wa bidhaa mbalimbali za mazao utafanywa na muuzaji ukishuhudiwa na mnunuzi.
		4	Bidhaa au Mazao yeyote yanayofungashwa kwa kutumia gunia ufungashaji wake usizidi mdomo wa gunia.
		5	Mtu yeyote atakayekiuka masharti ya kifungu hiki atakuwa ametenda kosa.
Ukaguzi wa vipimo na vifungashio	10	1	Wakala wa vipimo atakuwa na wajibu wa: - (a) Kukagua na kuthibitisha ubora wa vipimo vyote kabla ya kuanza kutumika na angalau kila baada ya mwaka mmoja baada ya kutumika kwa kipimo husika. (b) Kuweka alama maalum kuonyesha kuwa kipimo kimekakaguliwa.
		2	Afisa muidhiniwa akishirikiana na Afisa Mtendaji:- (a) Ataweza wakati wowote wa saa za kazi kuingia kwenye eneo lolote ambapo biashara ya mazao inafanyika kwa madhumuni ya kusimamia utekelezaji wa sheria ndogo hizi. (b) Atatembelea mara kwa mara maeneo ambayo biashara ya mazao inafanyika na kuhakikisha kuwa vipimo vyote vinavyotumika vimekaguliwa na wakala wa vipimo. (c) Ataweza kumchukulia hatua za kisheria mtu yeyote atakayevunja Sheria Ndogo hizi.
		3	Afisa muidhiniwa wakati wowote wa saa za kazi anaweza kuingia kwenye eneo lolote ambapo biashara ya mazao inafanyika kukamata na kuchukua vipimo au vifungashio vyote vitakavyobainika kukosa sifa ya kutumika kama vipimo au vifungashio halali kwa mazao husika.
		4	Itakuwa ni wajibu wa muuzaji na mmiliki wa kipimo kuhakikisha anapeleka kipimo kwa Wakala wa vipimo kwa ajili ya kukaguliwa angalau kila baada ya miezi kumi na mbili.
			SEHEMU YA TANO MAKOSA NA ADHABU

Makosa	11		Itakua ni kosa chini ya Sheria Ndogo hizi kwa mtu yeyote; (a) Kuuza au kununua mazao eneo tofauti na Gulio au Soko. (b) Kuuza au kununua mazao kwa kutumia vipimo visivyo halali. (c) Kutumia kipimo ambacho hakijaidhinishwa au kukaguliwa na Wakala wa vipimo. (d) Kumzuia afisa muidhiniwa kutekeleza wajibu wake kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi. (e) Udanganyifu katika matumizi ya kipimo. (f) Udanganyifu wa malipo ya ushuru (g) Kutoa taarifa ambazo anajua si za kweli.
Adhabu	12		Mtu yeyote atakayeshindwa au kukataa kutekeleza masharti ya Sheria Ndogo hizi atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyozidi shilingi elfu hamsini (50,000/=) na isiyopunga elfu thelathini (30,000/-) kwa kila kosa au kifungo kisichozidi miezi kumi na mbili (12) au vyote kwa pamoja faini na kifungo.

JEDWALI LA KWANZA

MAZAO MBALIMBALI NA JINSI AMBAVYO YANATAKIWA YAPIMWE

(Kifungu 9(1)(a)

(i) MAZAO YA MISITU

MAZAO	VIPIMO
Mkaa	Uzito
Mbao	Ujazo
Magogo	Ujazo
Fito	Urefu
Mianzi	Urefu
Asali	Uzito
Nguzo	Ujazo

(ii) MAZAO YA MASHAMBANI

MAZAO	VIPIMO
Mahindi punje	Uzito
Mpunga	Uzito
Viazi mviringo na jamii ya viazi	Uzito
Vitunguu maji/swaumu	Uzito
Ulezi	Uzito
Alizeti	Uzito
Pilipili hoho/mbuzi n.k	Uzito
Karanga	Uzito
Njegere mbichi	Uzito
Ngano	Uzito
Mtama	Uzito
Maharagwe	Uzito
Kunde na jamii ya kunde	Uzito
Mchele	Uzito
Korosho katika gamba	Uzito
Nyanya	Uzito
Ufuta	Uzito

(iii) BIDHAA ZA ZILIZOSINDIKWA

BIDHAA	KIPIMO
Unga wa mahindi/ pumba	Uzito

Unga wa Ngano	Uzito
Unga wa Mhogo	Uzito
Unga wa ulezi	Uzito
Mikate	Uzito
Kahawa	Uzito
Chai	Uzito
Kakao	Uzito
Pilipili (chill sauce)	Kwa ujazo hadi lita moja na kisha uzito
Nyanya (tomato sauce)	Kwa ujazo hadi lita moja na kisha uzito
Mafuta ya kula	Kwa ujazo hadi lita moja na kisha uzito

(iv) MAZAO YA MAJINI KAMA BAHARI, MITO, MAZIWA,MABWAWA n.k

MAZAO	VIPIMO
Dagaa	Uzito
Samaki	Uzito

JEDWALI NAMBA MBILI

UFUNGASHAJI MAZAO/BIDHAA KWA UZITO NA UJAZO HALISI

(Kifungu 8(1)(b)

NA	MAZAO/BIDHAA	VIPIMO
1	Mpunga	Kilo 75
2	Mahindi	Kilo 90
3	Ufuta	Kilo 90
4	Maharage	Kilo 90

5	Kunde	Kilo 90
6	Vitunguu	Kilo 70
7	Alizeti	Kilo 40
8	Njegere mbichi	Kilo 90
9	Mchele	Kilo 100
10	Unga wa mahindi	Kilo 80
11	Ulezi	Kilo 90
12	Jamii ya viazi	Kilo 100
13	Dagaa	Kilo 70
14	Mbao, magogo, nguzo	Mita za ujazo (m^3)
15	Jamii ya mazao ya shambani ambayo hayakuainishwa katika jedwali hili	Isizidi kilo 100
16	Pumba za mahindi/mpunga	Kilo 50
17	Karanga	Kilo 90
18	Unga wa mhogo	Kilo 60
19	Viazi mviringo	Isizidi Kilo 100
20	Ngano (punje, unga)	Kilo 90
21	Nyanya	Kilo 50
22	Mkaa	Kilo 30

Mhuri wa Halmashauri ya Wilaya ya Iringa umebandikwa katika sheria ndogo hizi kufuatia mkutano wa baraza la madiwani uliofanyika tarehe…….mwezi……2015 mbele ya ;

……
ROBERT MASUNYA
MKURUGENZI MTENDAJI HALMASHAURI YA WILWAY AYA IRINGA.

……
STEPHEN MHAPA
MWENYEKITI HALMASHAURI YA WILWYA YA IRINGA.

NAKUBALI

……
MHE. GEORGE B.SIMBACHAWENE (MB)
WAZIRI WA NCHI –OR-TAMISEMI

DODOMA,

TAREHE……..MWEZI……2017.